

Scarlet fever (Swahili)

Homa nyekundu katika watoto



Homa nyekundu ni maambukizi ya bakteria ambayo yanaweza kusababisha koo ya kuumia na wakati mwingine upele wa ngozi. Dalili hutokea wakati bakteria hutoa sumu ambayo huenea katika damu.

Ishara na dalili



Homa



Koo nyekundu yenye kuumia



Upele unaoanzia kichwani na shingoni na kusambaa mwilini, mikononi na miguuni. Inaonekana ndani ya masaa 24-hadi 48 na huisha ndani ya siku 3 hadi 4.



Ngozi inasikika kukwaruza, kama karatasi ya mchanga. Inaweza kubambuka (kama kuchomwa na juu) wakati upele unafifia, na mara nyingi hutokea kwenye mikono, miguu au kwenye nepi au sehemu za siri.



Ngozi inaonekana nyekundu na madoa mekundu yanayogeuka kuwa meupe inapobonyeza



Ulimi mwekundu na matuta, inaweza kuwa na kuonekana kama stroberi



Madoa meupe nyuma ya koo



Tezi za limfu zilizovimba kwenye shingo

Matibabu

Homa nyekundu hutambuliwa na daktari (GP) baada ya uchunguzi wa kimwili. Daktari anaweza kuchukua usufi wa koo ili kupima na atakuambia ikiwa vipimo zaidi vinahitajika.

Homa nyekundu hutibiwa na viuavijasumu vya penisilin (vidonge vinavyochukuliwa kwa mdomo) kwa siku 10. Inaweza kuchukua hadi masaa 48 kwa dalili kupata bora.

Ikiwa haitatibiwa, homa nyekundu inaweza kusababisha matatizo makubwa kama vile homa kali ya baridi yabisi - ugonjwa unaoweza kuathiri moyo, viungo, ubongo na ngozi - inayoweza kusababisha ugonjwa wa moyo wa rumatizimu (kuharibika kwa moyo). Hili ni tatizo lisilo la kawaida lakini kubwa kwa hivyo ni muhimu kwa mtoto wako kumaliza matibabu yaliyopendekeza kwa GP.



Utunzaji wa nyumbani

Hakikisha mtoto wako anapumzika sana na mpe paracetamol (Panadol au Dymadon) na ibuprofen (Nurofen) ili kumsaidia kudhibiti maumivu au homa yoyote. Fuata maelekezo kwenye chupa au paketi kwa kipimo cha sahihi. Usimpe zaidi kuliko kiasi kilichopendekezwa kwa siku.

Mpe mtoto wako vinywaji vyenye sukari kama vile juisi, maziwa au elektroliti (zinazopatikana kutoka kwa duka lako la dawa). Ikiwa mtoto wako anakunywa nya kutosha, mkojo wake utakuwa na rangi ya manjano hafifu.

Mtoto wako atahitaji kuanza kutumia dawa za viuavijasumu zaidi ya siku 2 kabla ya kurudi shulenii au huduma ya kulea watoto. Anapojisikia mwenye afya, anaweza kurudi shulenii au huduma ya kulea watoto.

Ni muhimu kuosha mikono yako/ya mtoto wako na kitu chochote mtoto wako anachotumia kula na kunywa ili kuzuia kuenea kwa maambukizi.

Kwa ushauri wa matibabu usio wa dharura, piga simu 13 HEALTH (13 43 25 84) kuzungumza na muuguzi aliyesajiliwa saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki kwa gharama ya simu ya mtaa.



Omba kupata mkalimani ikiwa unamhitaji.

Wakati wa kuonana na daktari

Mwona GP wako ikiwa mtoto wako:

- anasikia maumivu, ingawa anachukua paracetamol au ibuprofen
- hataki kunywa chochote
- hajakojoa sana
- haipati nafuu.

Imeandaliwa na Idara ya Dharura, Hospitali ya Watoto ya Queensland. Tunatambua mchango wa watumiaji na walezi.

Resource ID: FS355. **Reviewed:** July 2022

Kanusho: Maelezo haya yametolewa na wataalamu wa afya kama mwongozo pekee na yanalenga kusaidia, si kubadili nafasi, majadiliano na daktari wa mtoto wako au wataalamu wa afya. Taarifa husashwa kila mara, kwa hivyo tafadhalii angalia kuwa unarejelea toleo la hivi majuzi zaidi. Tafuta ushauri wa matibabu, inapofaa, kwa wasiwasi kuhusu afya ya mtoto wako.